



**SHULE YA SEKONDARI THEMI HILL
S.L.P 1164, TABORA**

SIMU NA: Mkurugenzi 0782 596 800/0754 488 434

Mkuu wa Shule 0759 642 337/0621 155 198

Makamu Mkuu wa Shule 0769 202 820

Email: themihill17@gmail.com Website: www.themihillschools.sc.tz

NduguMzazi / Mlezi wa

**KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI THEMI HILL
(BOARDING) - WASICHANA**

Hongera Mzazi kwani mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza 2020 katika shule ya sekondari **THEMI HILL**, iliyopo Ipuli, barabara ya kuelekea Nzega katika Manispaa ya Tabora.

Karibu tushirikiane kumtengeneza **Mtanzania mpya** kwa kumpatia mwanao elimu bora na stahiki. Mwanao awapo shulen i kwetu atalelewa katika **maadili** mema ya kitanzania. Atapewa elimu ya darasani kwa kufuata Mtaala wa Serikali. Atafundishwa na kuelekezwa kuweka katika vitendo yale atakayokuwa amefundishwa. Bila kuathiri Mtaala wa masomo ya sekondari mwanao atapatiwa **juzi mbalimbali** za kumuwezesha kumudu maisha atakapokuwa amehitimu masomo ya sekondari.

“Kusoma kwa bidii, kuelezea yale aliyosoma, kufanya majaribio darasani na katika maabara mbalimbali hapa shulen i kwa bidii juhudhi na maarifa ni kipaumbele”. Mwanao atafundishwa na kuelekezwa kuboea maeneo yatakayomjenga katika kuchagua fani yake katika maisha yanayokuja.

Ni vyema wewe na mwanao mkazisoma kwa uangalifu, mkazielewa na kuzikubali sheria zote ndipo msaini fomu hii mkiahidi kuheshimu na kufuata **KANUNI NA TARATIBU** za shule.

Shule itafunguliwa siku ya Jumatatu tarehe 06.01.2020 kwa kidato cha Kwanza, cha Pili, cha Tatu na cha Nne. Mwanao anaombwa kufika siku hiyo na vifaa vilivyooneshwatika barua hii. Muda wa kuripoti ni saa mbili asubuhi hadi saa kumi jioni.

.....
Michael Stephen Mambo

MKURUGENZI

AHADI YA MZAZI/MLEZI

Mimi..... Mzazi/Mlezi wa

Nimesoma kwa umakini sheria za shule ya sekondari **THEMI HILL** na kuzielewa na kuzikubali. Ninaahidi kushirikiana na uongozi wa shule kuhakikisha kuwa mwanangu atazingatia kwa makini kwa muda wote atakaokuwa mwanafunzi katika shule hii.

Nakubali kuwa iwapo mwanangu atashindwa kufuata taratibu za shule kama alivyoahidi na baada ya kupata maonyo na maelekezo ya waalimu na walezi wake, pia iwapo atashindwa kufanya bidii katika masomo na kupata wastani unaokubalika Ambao ni asilimia sitini (60%) katika masomo yote mwisho wa muhula niko tayari aachishwe masomo katika shule ya sekondari THEMI HILL.

Ndimi wako..... Sahihi

Tarehe..... Simu na

AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi mwanafunzi.....mbele ya mzazi/mlezi wangu.....

Nimesoma kwa makini na kuelewa sheria na taratibu zote za shule ya sekondary THEMI HILL. Naahidi kuzifuata taratibu na sheria zote za shule hii. Nitajitahidi kwa kadiri ya uwezo wangu wote kujifunza kwa bidii, juhudhi na maarifa kwa msaada wa walimu na wanafunzi wenzangu ili niweze daima kupata wastani wa asilimia sitini (60%) katika mitihani yangu kila mwisho wa muhula na mwisho wa mwaka; na endapo nistashindwa kutekeleza hayo niko tayari niachishwe masomo katika shule ya sekondari ya Them Hill.

Ninaahidi nitakuwa mtiifu na msikivu kwa taratibu na maelekezo yote ya shule. Nitaheshimu uongozi mzima wa shule walimu na wahudumu wote wa shule hii. Pia viongozi wa serikali na wanafunzi wenzangu wote.

Toa vivuli vya fomu hii

Nakala: Moja abaki nayo mzazi/mlezi,

Moja abaki nayo mwanafunzi,

Moja irudishwe shule.

MAHITAJI YA SHULE

i) **ADA YA SHULE**

Kila mwanafunzi anapaswa kulipa Ada ya shule kiasi cha Tshs 1,600,000/= kwa mwaka na italipwa kwa awamu **mbili** au **nne** kama inavyooneshwa kwenye jedwali hapa chini.

Awamu mbili	January	July
	800,000/=	800,000/=

Awamu nne	January	April	July	September
	400,000/=	400,000/=	400,000/=	400,000/=

ii) **MAHITAJI YA LAZIMA**

- a) Fedha ya matibabu Tshs 60,000 kwa mwaka (kila mwanafunzi) AU aje na **BIMA** yake ya afya.
- b) Vifaa vya ofisi Tshs 15,000/= kwa mwaka.
- c) Ugaguzi wa shule Tshs 5,000/= kwa mwaka.
- d) Maktaba Tshs 10,000/= kwa mwaka.
- e) Kitambulisho Tsh. 10,000/=
- f) Vifaa vya maabara 100,000/=
- g) Mahafali ya Kidato cha Nne Tshs 20,000/=

NB: Fedha zote zilipwe kwenye akaunti ya shule.

CRDB – Tabora THEMI HILL SCHOOL DEV. ACCOUNT A/C01J1084825800

EXIM BANK (TANZANIA LIMITED) – TABORA THEMI HIL SCHOOLS

A/C 0270000559

iii) **VIFAA VYA USAFI SHULENI**

- Kila mwanafunzi anatakiwa kuleta vifaa vya kufanya usafi awapo shulenii, na viwasilishwe ofisi ya Makamu Mkuu wa shule wakati wa kuwasili kwa mwanafunzi shulenii:
 - a) Jembe moja jipya na mpini wake
 - b) Fyekeo jipya lenye makali
 - c) Ndoo mbili zenye ujazo wa lita 10
 - d) Soft broom- 1, Hard broom 1, na Squizer 1

- iv) **MAHITAJI YA OFISINI**
- a) Mwanafunzi aje na barua ya uthibitisho na yenye mhuri kutoka kwa Mwalimu Mkuu wa shule alikomaliza darasa la saba. (Barua iwe na namba ya mtihani wa darasa la saba).
 - b) Aje na jalada spring file 1 kwa ajili ya kuhifadhia taarifa zake.
 - c) Aje na nakala 1 ya cheti chake cha kuzaliwa.
 - d) **Cheti cha Daktari:** Mwanafunzi aje na cheti cha Daktari kinachothibitisha afya yake. (Hii imeambatanishwa na fomu hii)
 - e) Aje na picha passport size 6 yenye background ya blue (avae shati jeupe)
- v) **VIFAA VYA DARASANI**
- a) Aje na daftari 20, (tunashauri counter book quire 3) penseli 10, box 1 la kalamu, rula ndefu 1 (30 cm), vifutio vikubwa 2 na mkebe wa hisabati (**Mathematical set**) 1.
 - b) Aje na begi dogo 1 la kubeba madaftari.
 - c) **Vitabu vya kujisomea:** mwanafunzi aje na vitabu binafsi vya kujisomea kama vipo. (Masomo: Mathematics, Physics, Chemistry, Biology, History, Geography, Civics, English, Kiswahili na French)
 - d) Aje na bahasha nne (4) saizi ya A4. Bahasha hizi ni kwa ajili ya kuwatumia wazazi/walezi maendeleo ya kitaaluma na tabia ya mwanafunzi.
 - e) Mwanafunzi anapaswa kuja na rimu 1 ya karatasi (atapaswa kuleta rimu kila nusu muhula)
 - f) Aje na karatasi za grafu (graph pad) 1
 - g) Aje na Box file 1 (kubwa) kwa ajili ya kuhifadhia mitihani na mazoezi mbalimbali ya darasani.
- vi) **MAHITAJI YA BWENI**
- (a) Aje na Godoro 1 (ukubwa $2\frac{1}{2}$) au alipie Tsh 65,000/=
 - (b) Neti 1 rangi nyeupe au alipie Tshs 10,000/=
 - (c) Aje na blanketi 1 (shuleni ni Tsh. 20,000/= kwa 25,000/=)
 - (d) Shuka 4 rangi ya pink au alipie Tshs 32,000/=
 - (e) Blue Band kilo 1 au alipie Tshs 9,000/= (hii huletwaka kila baada ya nusu muhula)
 - (f) Kila mwanafunzi anapaswa aliye Tshs 6,000/= kwa ajili ya vyombo vya chakula.
 - (g) Taulo 1 la kuogea
 - (h) Khanga au kitenge pea 1
 - (i) Tochi 1na saa ya mkononi 1
 - (j) Kandambili za kuogea pea 2, viatu vya wazi pea 1
 - (k) Vest nyeupe 4, nguo za ndani (chupi) angalau 10.
 - (l) Sanitary towels (pedi) angalau pakti 3

- (m) Miswaki 3, Dawa ya meno 250 grams, Mafuta ya kujipaka (ya mgando) kopo kubwa.
- (n) Kiwi gram 80 kopo 2, Brashi za viatu 2, kitana cha nywele 1
- (o) Sabuni ya kufulia miche 3, ya unga kilo 2 na sabuni za kuogea 5.
- (p) Sanduku imara la chuma lenye kufuli, kwa ajili ya kuhifadhi vitu vyake.

SARE ZA SHULE:

- i) **SARE ZA DARASANI**
 - Kila mwanafunzi anatakiwa kulipia bank **Tshs 128,000/=** kwa ajili ya kushonewa sare za darasani. Atapatiwa jozi mbili za sketi, mashati mawili, Tai mbili, sweta mbili na T-shirt zenyenye nembo ya shule mbili kwa ajili ya vipindi vya darasani.
 - Pia aje na full tracksuit, nzito – rangi ya Dark Blue au alipie Tshs 30,000/= (isiwe yenye kubana)
 - Kila mwanafunzi aje na pea 4 za soksi ndefu nyupe (stockings) na **viamu vyeusi vyenye Kamba** pea 2 au alipie Tshs 30,000/=.
- ii) **SARE ZA MICHEZO**
 - Kila mwanafunzi anatakiwa kulipa Tshs **25,000/=** kwa ajili ya sare za michezo.
 - Aje na raba pea 1 au alipie Tshs 15,000/= na soksi (stocking) rangi yoyote pea 2 kwa ajili ya michezo.
- iii) **SARE ZA KAZI (NJE YA MADARASA)**
 - Kila mwanafunzi anatakiwa kuja na Gauni 2 zenyenye marinda mengi, ndefu na ya heshima (nchi 5 kutoka magotini kwenda chini) material ya kunguru ya zambarau/pupple (drafti ya zambarau) au alipie Tshs 60,000/=
- iv) **SARE ZA KUTOKEA (SUNDAY OUTFIT)**
 - Kila mwanafunzi anapaswa kuja na suti nyeusi, blouse ya mikono mifupi yenye vishikizo mbele na sketi ndefu ya mapande sita au alipie Tshs 60,000/=

Nguo zote za mwanafunzi ziandikwe majina yake kwa kutumia uzi

❖ Kumbuka:

- Hakikisha mwanao anayo namba ya mzazi/mlezi kwa ajili ya mawasiliano kati ya shule na wewe mzazi/mlezi

MWONGOZO WA KUJIUNGA NA THEMI HILL SECONDARY SCHOOL

AFYA:

- (i) Mwanafunzi anapaswa awe na afya nzuri ili aweze kusoma vizuri.
- (ii) Mzazi ahakikishe mtoto wake amepimwa afya na daktari na afike na cheti cha uthibitisho wa afya yake.
- (iii) **Mzazi/ mlezi asifiche ugonjwa wa mwanae** kwani inaweza kuhatarisha maisha yake.
- (iv) Shule hii haipokei kabisa mwanafunzi anayehitaji chakula maalum ‘special diet’.
- (v) Ni wajibu wa kila mwanafunzi kujilinda afya yake kwa kuzingatia kanuni zote za afya ikiwa ni pamoja na usafi wa mwili, mavazi na mazingira yanayomzunguka.

TAALUMA:

- i) Mwanafunzi anapaswa kuhuduria vipindi vyote vya darasani na kuandika muhtasari na kufanya kazi zote za darasani apewazo na walimu wake.
- ii) Mwanafunzi atawajibika kufanya mazoezi na mitihani yote inayotolewa darasani kwa wakati uliopangwa. Kila mwanafunzi anapaswa kujiunga katika vikundi vya majadiliano wakati wa ziada wa kujisomea.
- iii) Ni wajibu wa mzazi kupata au kudai ripoti ya maendeleo ya mtoto wake kila baada ya muhula wa masamo.
- iv) Mwanafunzi atakayeshindwa kuhuduria masomo darasani mfululizo wa siku saba bila maelezo ya kutosha atajiachisha masomo.
- v) Kila mzazi atawajibika kulipa ada kwa wakati.
- vi) Kila mwanafunzi anapaswa kujitahidi katika masomo yote na kufikia wastani wa shule yaani alama 60%.
- vii) Lughya inayotumika hapa shulenii KIINGEREZA au KIFARANSA tu. Lughya ya Kiingereza na Kifaransa inatumika nje na ndani ya darasa isipokuwa wakati wa somo la Kiswahili na Dini tu. Sheria hii inatiliwa mkazo sana. Mwanafunzi anayefanya makusudi kutofuata agizo hili atapoteza nafasi yake ya kuendelea na masomo katika shule hii kwani atashindwa kumudu masomo.

USAIFI

- i) Kila mwanafunzi analazimika aonekane nadhifu kimwili na kimavazi.
- ii) Mwanafunzi anatakiwa daima kuvaare sare ya shule wakati wote wa masomo na atapotoka nje ya shule. Baada ya masomo atavaa sare ya bweni. Hivyo afike na sare ya shule ya msingi aliyokuwa anasoma, na nguo moja ya kubadili wakati akisubiri sare ya shule na ya bweni.
- iii) Kila mwanafunzi awe na nywele fupi zilizochanwa vizuri na kucha ziwe fupi na zisipakwe rangi.

- iv) Mwanafunzi haruhusiwi kuvaahereni, bangili, mkufu, pete na mapambo mengine wala kupaka wanja na vipondozi vikali.
- v) Mavazi ni lazima yawe na urefu wa kutosha safi na nadhifu.
- vi) Kila mwanafunzi atawajibika kutunza vifaa vyake binafsi mfano mavazi, daftari, vitabu, vifaa nya shule atakavyokabidhiwa mfano:- kitanda, dawati, kiti, godoro n.k.
- vii) Ni wajibu wa mwanafunzi kutunza mahali anapolala, kufanya usafi wa bweni na kupanga vifaa vyake vizuri. Ni wajibu wa mwanafunzi kutunza mazingira ya njie na ndani ya darasa. Ni marufuku wanafunzi kutupa taka au karatasi ovyo ndani ya darasa au katika viwanja nya shule.
- viii) Kila mwanafunzi atawajibika kutunza vyombo na mazingira ya shule mfano, kuta za majengo, madirisha, kabati n.k. iwapo ataharibu chochote atalazimika kufidia chombo kingine kuonesha ukomavu kimaadili.

NIDHAMU

- a) Kila mwanafunzi atawajibika kutii sheria na taratibu zote halali za shule zinazotolewa na uongozi mzima wa shule kwa mfano Mkuu wa shule, waalimu, viongozi wa Baraza la wanafunzi na wahudumu wengine wote. Kushindwa kufanya hivyo adhabu ya kosa la kwanza ni kusimamishwa masomo kwa wiki mbili.
- b) Ni marufuku mwanafunzi kutumia lugha zisizofaa mfano matusi, maneno ya dharau na kebehi kwa kutamka au kuandika dhidi ya uongozi wa shule, waalimu, viranja, wahudumu wengine au wanafunzi wenzake.
- c) Ni marufuku mwanafunzi kutumia jina tofauti na lililoandikwa katika orodha ya kujiunga na shule hii wakati wowote.
- d) Mwanafunzi analazimika kuandika jina lake katika vitu vyake vyote atakavyokuja navyo, hii ni pamoja na nguo zake binafsi, ndoo, jembe, fyekeo nk.
- e) Kila mwanafunzi anawajibika kuonesha adabu njema kwa watu wote wakubwa kwa wadogo, viongozi na wenzake bila hofu au unafiki.
- f) Kila mwanafunzi aonyeshe nidhamu katika kuvaahereni na mwenendo wake mzima.
- g) Kila mwanafunzi atalazimika kuwahi shulenii, darasani na kila mahali anapotakiwa.
- h) Kila mwanafunzi anawajibika kutii kengele na kuwahi popote anapotakiwa.
- i) Wanafunzi wote wataanza shughuli zote za siku kwa sala. Tunaamini kuwa sala zinampatia kila mmoja neema na baraka katika yote atakayofanya kwa siku nzima.
- j) Mwanafunzi haruhusiwi kuja na vyombo nya muziki kama radio au chochote kifananacho na hicho. Hairuhusiwi pia kuja na heater au simu ya mkononi.

SHERIA MUHIMU ZA SHULE

Hizi ni sheria ambazo ni sharti zifuatwe na kila mwanafunzi wa shule hii. Kwa hiyo Mzazi/Mlezi na mtoto wake wazisome kwa makini na wazikubali kwanza kabla ya mtoto kufika katika shule hii. Sheria za shule hii ni dira ya kukuwezesha kuwa na uhakika wa mwenendo wako katika safari yako ukizifuata vizuri utafanikiwa kufika mwisho wa safari yako.

- 1) Kwa ajili ya utaratibu na mafanikio mema katika masomo na malezi mema mwanafunzi anahitajiwa kuwa na adabu na heshima kwa watu wote wakati wote.
- 2) Shule hii hupokea wanafunzi wa dini na madhehebu mabalimbali ya dini, kwa hiyo ni lazima wote waheshimiane bila kubaguana. Ibada na sala zitafanyika kwa pamoja.
- 3) Kila mwanafunzi afahamu kwamba anaingia hapa kujifunza na kujenga utu wema kama maandalio ya maisha ya baadaye. Apewapo kazi yoyote aifanye kwa moyo na kwa wakati na namna ilivyopangwa **bila kufuatwa na kusimamiwa**. Akiwa na shida inayomfanya ashindwe kutekeleza wajibu wake ipasavyo ajieleze kwa viongozi wa ngazi zote. Akichelewa kufanya hivyo atachukuliwa hatua hata kama alikuwa na sababu za kutosha kushindwa kutekeleza wajibu wake.
- 4) Maadamu tunaelewa wazi kwamba elimu ni kazi, wanafunzi wanapaswa kujenga moyo wa kupenda, kuthamini na kufanya kazi za mikono kwa juhudhi na maarifa. Afahamu kwamba kazi za nje zinapewa uzito sawa na masomo ya kinadharia darasani. Awahi mahali pa kufanya kazi hiyo kwa moyo.
- 5) Kila mwanafunzi awe radhi kulelewa na kuelekezwa ifaavyo ili awe mlezi bora wa Tanzania ya kesho. Hivyo atunze na kuhifadhi mali yake mwenyewe, mali ya umma, kama majembe, mapanga, ndoo, vitanda, sahani, vikombe, madawati, viti, kuta, milango, sakafu na madirisha. Akiharibu kifaa chochote atapaswa kulipa.
- 6) Kabla ya kuingia katika shule hii mwanafunzi apimwe na aje na cheti cha daktari chenye kuthibitisha afya njema.
- 7) Hakuna ruhusa mwanafunzi kukaa na dawa bwenini. Dawa zote zikabidhiwe kwa matron au patron. Dawa za miti shamba haziruhusiwi shulenii.
- 8) Ni marufuku kabisa kwa mwanafunzi kulala bwenini saa za masomo au wakati wa kujifunza bila kutoa taarifa kwa wahusika. Taarifa hiyo aipate mwalimu wa zamu na mkuu wa shule mapema ili mgonjwa apatiwe huduma ipasavyo.
- 9) Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya eneo la shule bila kibali rasmi kutoka kwa Mkuu wa shule au Makamu wake kama yeye hayupo. Kibali hicho cha kutoka nje ya eneo la shule hakitolewi isipokuwa kwa sababu maalum.
- 10) Mwanafunzi akishafika shulenii asisumbue kuomba ruhusa kwenda nyumbani bila sababu maalum. Kama kuna sababu ya kutosha mzazi (baba au mama) afike shulenii kuomba ruhusa hiyo kwa utawala. Utawala ukiwa na sababu ya kutosha pia unaweza kumruhusu mwanafunzi aende nyumbani wakati wa masomo.

- 11) Hairuhuswi kuleta au kupokea vyakula kutoka kwa watu wa nje ya eneo la shule. Hii ni kwa usalama wa mwanafunzi asije akalishwa chakula kisichofaa.
- 12) Wanafunzi wote watakula chakula bwaloni kama familia moja na kama nafasi ya kujifunza adabu ya mezani. Kwa hiyo kila mwanafunzi ajue hairuhuswi kabisa kula chakula pengine. Kabla ya kula wanafunzi wote wanapaswa kusali.
- 13) Hairuhuswi kabisa kwa mwanafunzi kutembelea nyumba za wafanyakazi (waalimu na wasiowaalimu). Akilazimika kwenda huko aombe ruhusa kwa utawala.
- 14) Hairuhuswi wanafunzi kuingia jikoni, isipokuwa kwa ruhusa maalum.
- 15) Wageni hawaruhuswi kufika shulenii kuonana na wanafunzi wawapo masomoni, ikibidi kwa ajili ya tatizo kubwa kibali kitoke kwa Mkuu wa shule.
- 16) Taarifa zote muhimu toka kwa mzazi/mlezi mfano za vifo zipitie kwa mkuu wa shule
- 17) Wazazi watawatemebelea wanafunzi mara moja tu katika muhula itakayopangwa na uongozi wa shule.

MAKOSA YA KUJIFUKUZISHA SHULENI

Mwanafunzi atajifukuzisha shule mara ikiwa atatenda kinyume na maadili mema hasa katikamakosa yafuatayo:

1. Uasherati, uzinzi, usagaji.
2. Ulevi wa aina yoyote.
3. Wizi wa mali ya shule au ya wenzake
4. Kupigana au kutumia lugha chafu na ya matusi. Kuvuta sigara na kutumia madawa ya kulevya.
5. Kupata mimba, kutoa mimba
6. Kutoroka au kulala nje ya shule.
7. Kugoma au kuchochaea mgomo.
8. Kuharibu mali ya shule au ya wenzake kwa makusudi mfano: kuandika madawati, kuta, milango, vitabu vya shule, kuvunja swichi n.k.
9. Kupata ugonjwa wa zinaa kwa uthibitisho wa kukiuka namba 1
10. Makosa ya jinai kama vile: kujaribu kujiua, kutishia wengine kwa silaha kama kisu, nondo, bastola, sumu au kuua n.k
11. Kuiibia mtihani au kuchungulia majibu ya mtihani kwa wenzake na kuingia na karatasi zenye majibu ya mtihani au zilizoandikwa kwenye chumba cha mtihani.
12. Kila mwisho wa mwaka kutakuwa na mtihani maalumu wa kupanda au kuendelea darasa na atakayeshindwa kufikia wastani wa shule ambao ni 60% itampasa kurudia darasa hilo na akishindwa tena atakuwa amejifukuzisha shule mwenyewe.
13. Kudharau bendera ya Taifa, kudharau wimbo wa Taifa na nembo za Taifa.
14. Kudharau au kukufuru sehemu ya ibada ya dini au dhehebu lolote.
15. Kuolewa
16. Kuchelewa kufika shulenii tarehe iliyopangwa bila sababu maalum
17. Kukosa darasani au masomo kwa wiki moja bila sababu maalum.

MAKOSA AMBAYO YATASABABISHA MWANAFUNZI KUACHISHWA MASOMO
KWA MUDA MAALUM (SUSPENSION)

1. Kuchelewa darasani mara kwa mara.
2. Kukosa darasani mara kwa mara.
3. Kutokushiriki ibada mara kwa mara.
4. Kutofanya kazi za usafi na kazi za mikono mara kwa mara.
5. Kukwepa michezo mara kwa mara.
6. Kuonyesha kiburi, dharau na lugha ya matusi mara kwa mara.
7. Kupiga kelele mara kwa mara darasani na bwenini wakati wa kulala.
8. Kutofanya kazi za darasani wanazotoa waalimu.
9. Kukwepa majoribio ya darasani (test) na mitihani bila sababu maalum
10. Kutofuata taratibu zinazotakiwa wakati akiwa mgonjwa.
11. Kutowaa sare ya shule mara kawa mara
12. Kukosekana kwenye paredi ya kwanza na ya pili mara kwa mara.
13. Iwapo mwanafunzi ataachishwa masomo kwa muda maalum (suspension) ni lazima aende kwa wazazi/ walezi wake vinginevyo atakuwa amevunja sheria ya kukosa utii kwa wazazi/ walezi wake.

Mwanafunzi atakayeonesha tabia ya kurudia mara kwa mara makosa haya baada ya kuonywa, kupewa adhabu, kushauriwa na kusimamishwa masomo kwa muda maalumu, atakuwa amejifukuzisha shule mwenyewe.

Mwanafunzi ye yote mwenye maoni au malalamiko ayawasilishe kwa kiranja na vikao vya serikali ya wanafunzi na shule kwa kufuata ngazi au taratibu zilizowekwa. Migomo na fujo za aina yoyote haziruhusiwi kabisa.



THEMI HILL SECONDARY SCHOOL, P.O. BOX 1164, TABORA

PHONE: Director 0782 596 800/0754 488 434, Headmaster 0759 642 337/0621 155 198

To: The Doctor Concerned,

RE: MEDICAL EXAMINATION FORM

Please examine the following student and furnish me with his/her current health status. Requested by school authority

NAME: SEX:

ADDRESS:

OCCUPATION:

1. GENERAL EXAMINATION:

- (a) Ears:
- (b) Eyes:
- (c) Skin:
- (d) Upper and Lower extremities:
- (e) Chest:
- (f) Abdomen:
- (g) Dental:

2. PAST MEDICAL HISTORY:

3. LABORATORY EXAMINATION:

- (a) Urinalysis:
- (b) Stool:
- (c) Sputum:
- (d) B.S:
- (e) H.B:
- (f) Widal Test:
- (g) Pregnancy Test:

Remarks:

.....
.....
.....

Date:

Name: Title: Signature: